TANGAZO LA SERIKALI Na. 539M la tarehe 30/6/2024

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 27D)*

AMRI KUANZISHA HIFADHI YA TAIFA YA DHAHABU NA VITO YA MWAKA 2024

MPANGILIO WA AYA

*Aya* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito.
4. Madhumuni ya Hifadhi.
5. Vyanzo vya madini katika Hifadhi.
6. Usimamizi wa Hifadhi.
7. Bodi ya Usimamizi wa Hifadhi.
8. Majukumu ya Bodi.
9. Vikao vya Bodi
10. Malipo ya wajumbe wa Bodi.
11. Sekretarieti.
12. Ukaguzi.
13. Matumizi ya Hifadhi.
14. Zuio la matumizi ya Hifadhi.
15. Amana ya madini.
16. Uuzaji wa madini.
17. Bima.

SHERIA YA MADINI,
(SURA 123)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 27D)*

AMRI YA KUANZISHA HIFADHI YA TAIFA YA DHAHABU NA VITO YA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito ya mwaka 2024.

Tafsiri

**2**. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni Kamishna, Mkaguzi Mkuu, Mkaguzi, au afisa wa umma aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria au mtu aliyeteuliwa hivyo na Kamishna chini ya kifungu cha 25(2) cha Sheria au maafisa walioteuliwa na Wizara kusindikiza madini;

"amana" maana yake ni kuweka madini katika Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito kwa ajili ya kutunzwa;

Sura ya 197

"Benki" maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito;

"cheti cha madini" maana yake ni cheti cha amana ya madini au cheti cha uondoaji madini ambacho hutolewa na Tume ya Madini kwa Wizara na Benki kikieleza aina, thamani, kiasi na kiwango cha usafi wa madini yaliyowekwa au kutolewa;

"Hifadhi" maana yake ni Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito;

"madini" maana yake ni dhahabu na vito;

Sura ya 123

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Madini;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya fedha; na

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya fedha.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA HIFADHI

Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito

**3**. Inaanzishwa Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito ambayo itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Madhumuni ya Hifadhi

**4**. Madhumuni ya Hifadhi ni kuhifadhi dhahabu na vito kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya Taifa ya sasa, wakati wa hali ya hatari na mahitaji ya siku zijazo ili kuchangia kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Vyanzo vya madini katika Hifadhi

**5**. Vyanzo vya mapato ya Hifadhi vitakuwa-

(a) madini yaliyosafishwa yaliyolipwa kama mrabaha kwa mujibu wa matakwa ya Sheria;

(b) madini yaliyozuiliwa au kutaifishwa kwa mujibu wa sheria;

(c) madini yaliyonunuliwa na Serikali kwa mujibu wa masharti ya sheria;

(d) madini yaliyolipwa kama gawio chini ya utaratibu au makubaliano yoyote; na

(e) madini yaliyopatikana vinginevyo na Serikali.

Usimamizi wa Hifadhi

**6**.-(1) Waziri atakuwa na jukumu la jumla la usimamizi wa utendaji wa Hifadhi.

(2) Waziri atapokea taarifa kutoka kwa Bodi ya Taifa ya Hifadhi ya Dhahabu na Vito kwa ajili ya kumbukumbu, idhini au kutoa mwongozo.

(3) Benki Kuu ya Tanzania itakuwa na wajibu wa-

(a) kudhibiti na kusimamia Hifadhi;

(b) kuhifadhi dhahabu na vito vyote vilivyowekwa kwenye Hifadhi; na

(c) kumshauri Waziri na Bodi katika masuala yote yanayohusu usimamizi madhubuti wa Hifadhi.

Bodi ya Usimamizi wa Hifadhi

**7**.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Usimamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Dhahabu na Vito ambayo itakuwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Waziri na wajumbe wengine tisa.

(2) Wajumbe wa Bodi watateuliwa na Waziri kutoka Ofisi ya Rais, Wizara yenye dhamana ya fedha, Wizara yenye dhamana ya madini, Wizara yenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Benki Kuu na Tume ya Madini.

(3) Mtu atakayeteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi atapaswa kuwa na ujuzi, utaalamu na uzoefu katika fani za madini, fedha, usimamizi wa uwekezaji, sheria au fani nyingine yoyote inayohusiana nayo.

(4) Mjumbe wa Bodi atashika nafasi kwa muda wa miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja zaidi.

Majukumu ya Bodi

**8**.-(1) Majukumu ya Bodi yatakuwa ni-

(a) kuhakikisha ukuaji na uendelevu wa Hifadhi;
(b) kuandaa, kujadili na kumshauri Waziri kuhusu mikakati ya uwekezaji wa Hifadhi, pamoja na kusimamia utekelezaji wa mikakati husika;
(c) kupitisha na kuwasilisha kwa Waziri taarifa za nusu mwaka za utendaji wa Hifadhi;
(d) kupendekeza utoaji na kuweka utaratibu wa uuzaji wa madini; na
(e) kutoa maelekezo kwa Benki juu ya usimamizi madhubuti wa Hifadhi kadri itakavyoona inafaa.

(2) Majadiliano ya Bodi yatazingatia-

(a) lengo la jumla kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo vya Jamhuri ya Muungano;
(b) hali ya sasa ya kiuchumi, fursa na vikwazo katika masoko ya uwekezaji na vikwazo vinavyoikabili Benki na taasisi nyingine katika utendaji; na
(c) uendelevu wa Hifadhi pale inapotokea haja ya mabadiliko ili kukidhi upungufu usiotarajiwa wa mapato ya madini.

Vikao vya Bodi

**9**.-(1) Bodi itakutana mara moja katika kila robo mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake.

(2) Akidi katika kikao itakuwa ni wajumbe saba.

(3) Uamuzi wa Bodi utafikiwa kwa maridhiano.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya aya ndogo ya (3), iwapo wajumbe wa Bodi watashindwa kuafikiana juu ya suala lolote, suala hilo litaamuliwa kwa kura na ikiwa kura zitalingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi zaidi ya kura yake ya awali.

Malipo ya wajumbe wa Bodi

**10**. Wajumbe wa Bodi watalipwa kwa mujibu wa miongozo ya malipo itakayotolewa na Benki.

Sekretarieti

**11**. Benki itakuwa Sekretarieti ya Bodi.

Ukaguzi

**12**. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua shughuli za Hifadhi.

Matumizi ya Hifadhi

**13**.-(1) Waziri, baada ya kushauriana na Bodi, anaweza kuidhinisha matumizi ya Hifadhi.

(2) Bila kuathiri aya ndogo ya (1), matumizi ya Hifadhi yatakuwa kwa ajili ya -

(a) ununuzi wa dhahabu au vito ili kuimarisha Hifadhi; na

(b) kufadhili matumizi ya Serikali katika hali ya hatari baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri.

Zuio la matumizi ya Hifadhi

**14**. Hifadhi itatumika kwa lengo lililokusudiwa katika Amri hiii.

Amana ya madini

**15**.-(1) Pale ambapo Wizara inakusudia kuweka amana kwenye Hifadhi itaitaarifu Benki kwa maandishi.

(2) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (1), taarifa kutoka Wizarani-

(a) itasainiwa na afisa aliyeidhinishwa na Wizara;

(b) itawasilishwa angalau siku moja ya kazi kabla ya siku ya kuweka amana;

(c) itaonesha kundi, aina, kiasi na kiwango cha usafi wa madini yaliyokusudiwa kuwekwa

kwenye Hifadhi;

(d) itaonesha majina ya maafisa walioidhinishwa kutoka Wizarani na Tume ya Madini walioteuliwa kusindikiza madini hayo.

(3) Afisa aliyeidhinishwa wa Tume ya Madini atafungua mzigo wenye madini kwa madhumuni ya kufanya uhakiki wa madini kwa lengo la kuthibitisha uhalisia wake.

(4) Tume ya Madini itahakikisha kuwa kuna maafisa walioidhinishwa katika uhakiki wa madini kulingana na mazingira ili kulinda uadilifu wa mchakato huo.

(5) Baada ya kukamilika kwa taratibu za kuweka amana, Tume ya Madini itatekeleza na kutoa cheti cha madini katika fomu itakayoainishwa na Benki.

Uzaji wa madini

**16**.-(1) Bodi, baada ya kupata kibali cha Waziri, inaweza wakati wowote kuuza kiasi madini yaliyo kwenye Hifadhi.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1), Bodi haitauza kiasi chote cha madini kilichopo kwenye Hifadhi.

(3) Kwa kuzingatia masharti yaliyotangulia ya aya hii, katika uuzaji wa madini yaliyowekwa kwenye Hifadhi, Benki itakuwa na haki ya kwanza ya kununua madini.

Bima

**17**.-(1) Bodi itakata bima kwa ajili ya madini wakati wa kusafirishwa na katika kipindi yatayokuwa yametunzwa katika Hifadhi.

(2) Kwa madhumuni ya aya ndogo ya (1), Benki baada ya kushauriana na Wizara, itafanya uamuzi kuhusu bima inayofaa kwa ajili ya madini.

Dodoma,
30 Juni, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*